

HUYU NI KAKA

- | | |
|--|--|
| <p>1. Ni mahiri kwa kuamba, na kulaghai kibara.
Kwa mwendo huo sambamba, na nyingi mno hasara.
Sana huweka kizimba, na kushawishi madhara.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> <p>2. Mtu kujenga nyumba, si kwamba kujikadara.
Ni kazi huko kupamba, au kuziba zingira.
Ela haya ni mabamba, kuyafanyiwa bara bara.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> <p>3. Kwamba hii yangu kamba, sitaki ije dorora.
Nakazia penye nyumba, wote na wakining'ara.
Ghiba kumpa kibamba, hohe hahe mwenye bara.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> | <p>4. Utasilikwa eh! mwamba, huku mambo yatatira.
Akioga huyo mwamba, bila tashwishi kujira.
Huku nyimbo akiimba, penzi kufanya imara.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> <p>5. Hutenda kwa kujigamba, kama yeye si asira.
Kila aali ya nyumba, hupewa bila papara.
Nakwambia haya imba, dhikiri ndugu dhikira.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> <p>6. Kwamba kuna kitu mimba, ndiyo yaanza kujira.
Haifai ukiimba, ili uone taswira.
Iwapo kutwa huvimba, utaona yake sura.
Hali hiyo inang'ara, bila mtu kuibamba.</p> |
|--|--|

Hamidu R. Tambwe
Julai, 1970.